

25/01/2024

## **Tukio la ‘Red Table Talk’ Lakuza Umoja na Uelewano Miongoni mwa Wanawake Vijana katika Southwest DeKalb High**

*Kuadhimisha Siku ya Waanzilishi, Wanachama wa Delta Sigma Theta Waonyesha Nguvu ya Udada*

Baada tu ya kuanza kwa mwaka mpya, Januari katika Southwest DeKalb High School imekuwa wakati wa kukuza udada na uwezeshaji. Tukio la pili la *Red Table Talk* la kila mwaka katika shule hii liliandaliwa tarehe 11 Januari kama sehemu ya sherehe za Siku ya Waanzilishi wa vyama vya udada na udugu vya Watu Weusi. Lengo la tukio hili lilikuwa kufundisha wanawake vijana umuhimu mkubwa wa kuwa na umoja na ushirikiano.

Tukio liliandaliwa na wanachama 22 wa Delta Sigma Theta Sorority wa shule hii, na mada ya mwaka huu ilikuwa *In Search of Sisterhood (Kutafuta Udada)*, na kuongoza shughuli kwa wanafunzi 44 walioshiriki kuanzia gredi za 9 hadi 12. Kupitia mazungumzo na michezo, wanafunzi walijifunza kuhusu manufaa ya kimaisha ya kushirikiana kama timu.

“Tulitaka kuandaa mpango wa ushauri ili kuwasaidia wasichana kuhusiana na kanuni za udada na umoja na kuwafundisha jinsi ushirikiano unavyofanya kila jambo kuwa bora zaidi,” alisema mwalimu wa Kiingereza Dkt. E. Yvette Walters. “Tukio la *Red Table Talk* lilianzishwa ili kukuza udada kati ya wanawake wadogo katika Southwest DeKalb High School.”

Mwaka jana, kusudi la mkusanyiko huo lilikuwa kuwafahamisha wanafunzi kuhusu mipango ya shule za upili inayopatikana kupitia chama cha Delta Sigma Theta. Ilikuwa dhahiri kuwa kuna maendeleo maalum yaliyokuwa yakifanyika. Wasichana, wakiwa wamegawanywa katika makundi, walishiriki katika majadiliano ya maana na michezo shirikishi, kuvunja vizuizi na kujenga mahusiano, kuleta athari kwa washiriki wanafunzi.

“Lilikuwa tukio la kuelimisha kwa kujifunza kuzoea na kushirikiana na watu tofauti na kuelewa umuhimu wa kuweka kando ubinafsi ili kufanya kazi ya pamoja,” Carrington Howard, mwanafunzi wa mwaka wa mwisho wa shule ya upili alisema.

Umuhimu wa tukio hili ni zaidi ya sherehe za kila mwaka; ni kuahidi kujitolea kwa maadili ya chama kuhusu udada, masomo, huduma na hatua za kijamii.

“Kuwarezesha wasichana hawa ni muhimu, haswa sasa. Inahusu kuwafundisha kutegemeana iwe ni wakati wa raha au wa shida, kukuza jamii inayosaidiana,” Dkt. Walters alielezea.

Mshauri wa shule Imani Handy alikubaliana, “Tukio hili ni njia yetu ya kuwasaidia wengine, kwa kulenga elimu na jamii.”

Kama unavyoona, tukio la “*Red Table Talk*” katika Southwest DeKalb High School limekuwa zaidi ya tukio la kawaida. Limekuwa somo la kila mwaka kuhusu umoja, kusherehekea utofauti, na ushuhuda wa nguvu inayopatikana katika udada. Masomo haya yanaweza kuwasaidia katika panda-shuka za kimaisha.